



**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA: KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA ZA KISHERIA KWA WAGUSWA WA UTWAAJI WA ARDHI YA MKUZA WA BOMBA LA MAFUTA KATIKA MRADI WA EACOP.
KUMBUKUMBU NA.0010007423**

Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Total Energies East Africa Midstream B.V. ya nchini Tanzania, inakaribisha watoa huduma wenye uzoefu na sifa kuonesha nia yao kwa ajili ya utoaji wa huduma za kisheria kwa waguswa wa utwaji wa Ardhi ya Mkuza wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:

Mradi wa EACOP unatafuta kampuni ya uwakili iliyo na uwezo wa kutoa ushauri na usaidizi kwa Watu Walioguswa na Mradi (PAPs) wakati wa mchakato wa utwaji wa ardhi kwa ajili ya Mkuza wa Bomba la mafuta. Ushauri na usaidizi unaohitajika utalenga taarifa za stahiki, mchakato wa mkataba wa fidia (EBCA) kwa muda wa miezi 3 baada ya malipo ya fidia kufanyika. MZABUNI ataanzisha madawati ya muda ya msaada katika vijiji vilivyoguswa na utwaji wa ardhi kwa ajili ya mkuza wa bomba la mafuta na kuwapatia washauri wenye sifa na waliosajiliwa. Washauri hawa watakuwa na ufahamu katika sheria ya Tanzania ya utwaji ardhi na taratibu zinazohusiana. Huduma hizo za ushauri zitatolewa bure kwa PAPs.

VIGEZO MUHIMU:

Kampuni za uwakili zinazoonyesha nia zinaalikwa kutuma maombi yao huku zikiambatanisha:

- Uthibitisho wa usajili ikiwa ni pamoja na leseni ya sasa ya biashara.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Cheti cha mlipa kodi ya mapato (TRA) cha mwaka wa hivi karibuni.
- Wakati wa kuwasilisha majibu kuonesha nia unasisitizwa sana kuambatisha maombi ya kujisajili kwenye kazi data ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma wa Ndani.
- Kukidhi vigezo na Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa Vyeti vya kutoa huduma na shughuli za kisheria vya sasa.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya tarehe **9 Februari 2022** saa **11 jioni** saa za Afrika Mashariki (EAT), Barua pepe inapaswa kuwa **0010007423**.

Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Maombi yote ya kuoresha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.